November 2015 subject reports

# Swahili B

## Overall grade boundaries

### Higher level

| Grade: | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mark range: | 0 - 14 | 15 - 29 | 30 - 45 | 46 - 58 | 59 - 70 | 71 - 84 | 85 - 100 |

### Standard level

| Grade: | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mark range: | 0 - 12 | 13 - 25 | 26 - 43 | 44 - 59 | 60 - 74 | 75 - 87 | 88 - 100 |

## Higher level internal assessment

### Component grade boundaries

| Grade: | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mark range: | 0 - 3 | 4 - 6 | 7 - 12 | 13 - 17 | 18 - 21 | 22 - 26 | 27 - 30 |

As there were very few candidates entered for HL this session, it is inappropriate to draw conclusions on candidate performance.

## Standard level internal assessment

### Component grade boundaries

| **Grade:** | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mark range:** | 0 - 3 | 4 - 6 | 7 - 12 | 13 - 17 | 18 - 21 | 22 - 26 | 27 - 30 |

## Kiwango na ufaafu wa kazi iliyowasilishwa

Kazi hii ilikuwa ya wastani na iliwafaa wanafunzin katika kiwango hiki. Wanafunzi wote walifanya vyema. Sehemu zote mbili za kazi hii zilikuwa zinaeleweka vizuri na wanafunzi. Walimu waliwashirikisha wanafunzi kama ipasavyo. Walimu pamoja na wanafunzi walitumia muda vizuri kama ilivyo katika maagizo. Karatasi hii ni muhimu sana kukuza lugha ya wanafunzi katika mazungumzo na kuwapa uwezo wa kuwasilisha mada tofauti. Walimu walikuwa wamewatayarisha wanafunzi vilivyo, na pia wanafunzi walidhihirisha hayo katika mawasilisho yao. Ni kazi inayowapa watahiniwa nafasi ya kufikiria kwa kina na kutoa hoja zao ambazo wamebuni wenyewe wakizingatia mada ambazo wameshughulikia darasani pamoja na walimu wao.

## Utendaji wa mtahiniwa dhidi ya kila kigezo

Wanafunzi walifanya vyema katika kila kigezo. Uwezo wa kueleza picha walizopewa ulikuwa wa hali ya juu. Wanafunzi waliweza pia kushiriki na kuendeleza mazungumzo huku wakiongozwa na walimu wao wakihimizwa watoe maoni au kujibu maswali walioulizwa kwa kina. Kila mwanafunzi aliweza kuhusisha picha na maandishi yaliyokuwa chini yake pamoja na mada walizokuwa wameshughulikia katika masomo yao; kama vile:afya, mazingira, utamaduni na kadhalika. Matumizi ya lugha yalikuwa ya hali ya juu kwa wanafunzi wengi isipokuwa wachahche waliokuwa na ugumu wa msamiati na upatanisho wa ngeli. Mawazo yaliyokuwa kwenye picha yalisawiriwa vyema na wanafunzi wengi. Wakati mwingine ugumu ulitokea pindi tu hoja tofauti na maandishi yaliyoandamana na picha zilipojumuishwa katika mazungumzo na mwalimu. Sehemu iliyohitaji wanafunzi kutanguliza picha na kuzihusisha na mada fulani hazikuwatatiza wanafunzi; ithibati kuwa walikuwa na ustadi wa mada tofauti pamoja na matumizi ya lugha.

## Mapendekezo na mwongozo wa kufundisha watahiniwa wa siku sijazo

Ningependekeza picha zote wanafunzi walizoulizwa kuwasilisha kuhusu ziwe na maandishi ya kuwaelekeza wanapowasilisha. Kuna picha ambazo hazikuwa na maandishin yoyote ambayo yangekuwa muhimu ili kuwasaidia wanafunzi kupata habari na kupata angalau kidokezo na habari za picha kwa jumla. Ni vizuri pia kuepuka mtindo wa ‘swali-jibu’ kutoka mwanzo hadi mwisho wa wasilisho. Ni vyema walimu kujumuisha kauli ambazo wanafunzi watatoa maoni kuhusu, sio tu maswali ya kujibiwa. Mazoezi ya mara kwa mara yatawafaa wanafunzi kwa


International Baccalaureate® Baccalauréat International Bachillerato Internacional

kujiandaa na kupata uzoefu wa kukabiliana na mtihani wa aina hii. Mazoezi pia yatawapa wanafunzi ujasiri wa kushiriki na kuendeleza mazungumzo bila woga au kusitasita.

## Maoni mengine

Watahiniwa wote walifanya kazi nzuri. Ni njia nzuri ya kukuza uwezo wa wanafunzi wa lugha katika mazungumzo. Ni vyema kila mwanafunzi apate muda wake wa kuwasilisha kama ilivyopendekezwa katika maagizo. Kuna mwanafunzi mmoja hakupewa muda wa kutosha kuwasilisha. Aliwasilisha kwa muda wa chini ya dakika tano ilhali wengine walipata muda wa dakika nane hadi kumi. Ni vyema pia mwalimu kusubiri mtahiniwa amalize kauli moja kabla ya kuuliza swali lingine. Kuna kisa kimoja au viwili mwalimu alimkatiza mwanafunzi na kumuuliza swali lingine hata kabla ya kujibu swali la hapo awali.

## Higher level written assignment

### Component grade boundaries

| **Grade:** | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mark range:** | 0 - 4 | 5 - 8 | 9 - 12 | 13 - 15 | 16 - 17 | 18 - 20 | 21 - 24 |

## Standard level written assignment

### Component grade boundaries

| **Grade:** | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mark range:** | 0 - 3 | 4 - 7 | 8 - 11 | 12 - 14 | 15 - 17 | 18 - 20 | 21 - 24 |

## Kiwango na ufaafu wa kazi iliyowasilishwa

Kazi zilizowasilishwa zinafaa kiwango hiki. Maelezo na maagizo ya kuwaelekeza wanafunzi kuandika insha hizi yanaridhisha. Muundo na mtindo wa uandishi wa insha za aina hii unawawezesha wanafunzi kuandika kazi ambazo zinafuata hatua kwa hatua. Sehemu ya kwanza inayotanguliza kazi, mada yake, umuhimu, na yaliyopo kwenye marejeleo ni mbinu muhimu ili watahiniwa wanapoanza kuandika kazi yenyewe wasipotoke na kwenda nje ya mada. Watahiniwa kupata uhuru wa kuandika kuhusu mada yoyote chini ya usimamizi wa walimu wao ni njia nzuri ya kuwapa nafasi ya kuandika mada wanazohisi wana uwezo nazo pamoja na upatikanaji wa marejeleo. Kwa sababu watahiniwa wana umaarufu tofauti katika


International Baccalaureate® Baccalauréat International Bachillerato Internacional

uandishi wa insha za tanzu tofauti, uhuru wa kuchagua utanzu mtahiniwa ana umahiri nao unawawezesha kutokuwa na vikwazo vyovyote, na hivyo kila mwanafunzi kupata nafasi ya kupata alama za juu. Muda wanaopata kufikiria, kuandaa, kuandika, kudurusu marejeleo, kutahmini na kusahihisha kazi zao wanafunzi kunawawezesha kuwa na wakati wa kutosha kuandika insha bora kadiri ya uwezo wa kila mwanafunzi.

## Utendaji wa mtahiniwa dhidi ya kila kigezo

Wanafunzi wengi walielewa kazi waliohitajika kufanya. Asilimia kubwa ilizingatia mpangilio wa insha wa kuitanguliza kwa umuhimu na lengo la kazi yenyewe na kisha kufuatwa na kazi iliyojumuisha maudhui pamoja na ujumbe uliotokana na matini zilizorejelewa. Idadi ya maneno katika sehemu zote mbili za insha ilizingatiwa kwa umakinifu. Mada ambazo wanafunzi walichagua ziliambatana na kuoana vizuri na kazi ambazo waliandika pamoja na marejeleo waliotumia. Hata hivyo, kuna wengine ambao hawakuweza kueleza mantiki vizuri katika sehemu ya kwanza kabla ya kutanguliza kazi yenyewe. Matumizi ya lugha kwa kiwango kikubwa yalikuwa yanafaa na wanafunzi pia walionyesha kuelewa ni nini walihitajika kufanya. Kuna wanafunzi wachahce waliokuwa na changamoto katika hijai na upatanisho wa ngeli. Matumizi ya lugha kulingana na kazi walizoandika wanafunzi yalikuwa sawa isipokuwa tu wachache tu.

## Mapendekezo na mwongozo wa kufundisha watahiniwa wa siku sijazo

Kuna wanafunzi walioonekana kama hawakuelewa kabisa yanayohitajika katika uandishi wa insha kama hii. Ningependekeza wanafunzi wa siku zijazo wawe wanaandika kazi kama hizi mara kwa mara hata kabla ya mtihani wenyewe. Mazoezi kama haya yatawawezesha wanafunzi kupata usaidizi kutoka kwa walimu jinsi ya kuunganisha marejeleo na kazi wanazoandika. Uzoefu huu utawawezesha wanafunzi kuongeza ujuzi wao wa jinsi ya koanisha utangulizi wa insha, marejeleo, na kazi yenyewe. Wanafunzi pia ni vizuri wahimizwe kuchagua mada ambazo wataweza kuzifanyia utafiti na kuandika kuzihusu ili kupunguza ugumu wakati wa mtihani.

## Maoni mengine

Hii ni kazi nzuri kwa wanafunzi kwani wanakuza uwezo wao wa kufanya utafiti wa kimaktaba na pia wanapata uwezo wa kuandika makala wakitumia makala nyingine pamoja na kujumuisha ujuzi wao wa mada husika. Uandishi huu unawatayarisha wanafunzi vizuri katika nyanja za utafiti watakazojihusisha nazo katika masomo na kazi za baadaye. Kwa jumla, wanafunzi walifanya vizuri na inaonekana walikuwa wameandaliwa vizuri.


International Baccalaureate
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

## Higher level paper one

### Component grade boundaries

| Grade: | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mark range: | 0 - 12 | 13 - 25 | 26 - 33 | 34 - 40 | 41 - 46 | 47 - 53 | 54 - 60 |

## Standard level paper one

### Component grade boundaries

| Grade: | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mark range: | 0 - 6 | 7 - 13 | 14 - 20 | 21 - 27 | 28 - 35 | 36 - 40 | 41 - 45 |

## Maoni ya jumla

Mtihani wenyewe ulikuwa wa wastani. Maswali yalikuwa ya kiwango mwafaka na vifungu vilieleweka. Matokeo ya mtihani yalikuwa ya wastani; kuna wale waliofanya vyema na kuna wale waliolemewa kidogo. Maagizo yote yanaeleweka vizuri kwa watahiniwa, na aina mbalimbali za maswali kama ilivyokuwa kwenye mtihani ni mbinu nzuri ya kuwawezesha wanafunzi wa viwango tofauti kimasomo kupata nafasi kufanya vyema katika sehemu mbalimbali walizokuwa na uwezo nazo.

## Sehemu za programu na mtihani zilizooenekana kuwatatiza wanafunzi

Maswali yaliyoonekana kuwa magumu ni yale yaliyokuwa na majibu ya kuchagua. Kwa mfano sehemu zile watahiniwa walihitajika kuchagua sehemu ya sentensi inayolingana na sehemu iliyotolewa. Maswali yaliyohitaji kuchagua kauli ambazo ni sahihi kulingana na kifungu yaliwatatiza wanafunzi wengine.Hata hivyo kulikuwa na maswali mengine yenye majibu ya kuchagua kutoka kwenye orodha na watahiniwa wengi waliyajibu kwa ufasaha. Sehemu nyingine iliyoonekana kuwa tatizo kwa wanafunzi ni maswali ambayo yalihitaji kuelewa kifungu kisha kujibu swali kwa kurejelea sentensi au kauli kutoka kwenye kifungu. Maswali ya msamiati pia yalikuwa na ugumu kwa kiasi fulani kwa wanafunzi wengine. Kwa jumla, maswali yaliyohitaji watahiniwa kuelewa na kufasiri kifungu ili kutoa majibu mwafaka yaliwapa changamoto. Wakati mwingine watahiniwa hawakuelewa ni kutoka sehemu gani hadi gani ya kifungu walihitaji

kuirejelea katika majibu yao; wengine waliongeza sehemu ambazo hazikuwa zinahitajika na wengine kuacha sehemu zinazohitajika ili jibu liwe kamili.

## Sehemu za programu na mtihani ambazo wanafunzi walionekana kuwa wemejitayarishia vyema

Maswali mengi ya kutaja sifa fulani au mambo fulani kulingana na kifungu hayakuwatattiza wanafunzi. Kwa mfano swali la kwanza na swali la kumi na saba. Maswali haya yalihitaji watahiniwa kurudi kwenye kifungu na kunakili majibu kama yalivyo katika kifungu. Huenda hata wanafunzi wakawa si kujitayarisha vizuri kwa maswali kama haya, lakini yalikuwa rahisi kwani majibu ya maswali haya yaliweza kunukuliwa moja kwa moja kutoka kwenye kifungu. Kilichohitajika ni kufahamu swali linarejelea sehemu au aya gani katika kifungu na kisha kudondoa jibu au majibu kulingana na swali. Wanafunzi wengi pia waliweza kuyajibu maswali yaliyohitaji kauli fulani kubainishwa kama ni kweli au la, na kisha kutoa ithibati. Isipokuwa swali la kumi na moja ambalo mtahini alitumia ukanusho na wanafunzi wengine hawakugundua na kujibu kuwa ni kweli badala ya kinyume chake, asili mia kubwa ilipata maswali ya sehemu hii. Sehemu nyingine ambayo wanafunzi walifanya vizuri ni ile ambayo watahiniwa walihitajika kukamilisha jedwali kwa kuonyesha nini/nani neno fulani linarejelea katika kifungu.

## Uwezo na udhaifu wa watahiniwa kwa maswali binafsi

Kila mtahiniwa alikuwa na uwezo wake tofauti kwa maswali binafsi. Asili mia kubwa ya watahiniwa walidhihirisha uelewa wa vifungu vyote na maswali yaliyofuata licha ya wengine kutoa majibu ambayo hayafai. Kufeli kwa maswali yaliyofuatwa na orodha ya majibu ili watahiniwa wachague jibu mwafaka ni ishara ya kuwa wengi walioanguka maswali haya hawakurejelea kifungu kwa mara nyingine ili kuchunja majibu ambayo hayana uwezekano wa kuwa sahihi. Katika maswali yaliyokuwa na kauli za wanafunzi kusema ni kweli au si kweli na kisha kutoa thibitisho, kuna wanafunzi wengi sana waliokosea kauli ambayo mtahini alikanusha neno moja tu. Si kwamba wanafunzi hawangekuwa na uwezo wa kujibu, lakini walisoma kwa haraka na kurukia tu kwenye jibu. Udhaifu ulioonekana kulemaza uwezo wa kupata majibu ulitokana hasa na kutoelewa swali au kifungu vizuri. Shida hii ilitokana na uwezekano wa wanafunzi kutorejelea kifungu kwa mara nyingine ili kukifahamu vizuri.

## Mapendekezo na mwongozo wa kufundisha watahiniwa wa siku sijazo

Kwa watahiniwa wa siku zijazo, ni vyema wafundishwe namna ya kukabiliana na maswali yaliyo na majibu ya kuchagua. Umuhimu wa kurejelea kifungu mara nyingi iwezekanavyo ni vizuri usisitizwa. Jinsi ya kuchuja majibu ambayo hayana uwezekano wa kuwa sahihi hadi mtahiniwa abaki na jibu lililo sawa ni mbinu nyingine wanafunzi wanafaa kufundishwa pindi tu wajipatapo katika hali ambayo swali limekuwa ngumu. Manufaa ya kila sehemu ya maswali kutoa maagizo ni aya gani mtahiniwa anafaa kurejelea ili kujibu swali fulani yanafaa kusisitizwa pia. Katika sehemu ya msamiati, ni uzoefu wa lugha tu utakaowawezesha kukabiliana na maswali ya aina hii; hivyo kupendekeza mazoezi kabambe upande wa wanafunzi.

## Higher level paper two

### Component grade boundaries

| Grade: | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mark range: | 0 - 4 | 5 - 10 | 11 - 16 | 17 - 22 | 23 - 29 | 30 - 35 | 36 - 45 |

## Standard level paper two

### Component grade boundaries

| Grade: | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mark range: | 0 - 3 | 4 - 6 | 7 - 11 | 12 - 15 | 16 - 19 | 20 - 22 | 23 - 25 |

## Maoni ya jumla

Maswali yenyewe yaliwafaa watahiniwa wa kiwango hiki. Wanafunzi wengi walifanya vizuri na kuelewa maswali hasa swali la hotuba na swali la kuandika barua kuhusu mtindo na mavazi miongoni mwa vijana. Hata hivyo, kulikuwa na changamoto kwa kiasi fulani hasa kwa swali lililohitaji kuandikiwa ripoti na lile la mahojiano. Maswali tofauti ya insha zinazoshughulkia tanzu mbalimbali ni mbinu nzuri ya kumwezesha kila mtahiniwa kuchagua insha atakayomudu na yenye ana uwezo nayo. Hili liliwawezesha wanafunzi kutofungika katika mada au swali moja la karatasi hii. Asilimia kubwa ni ile ilielewa na kufuata maagizo kulingana na kila swali. Walimu walikuwa wamewatayarisha wanafunzi vyema katika kazi hii.

## Sehemu za programu na mtihani zilizooenekana kuwatatiza wanafunzi

Sehemu iliyoonekana kuwa ngumu kwa watahiniwa ni ya ripoti na mahojiano. Wanafunzi wengi waliliepuka swali lililohitaji kuandikiwa ripoti. Kuna wale waliojaribu kuandika insha ya ripoti lakini si wengi walidhihirisha kuwa na ufahamu wa jinsi ya kuandika ripoti. Utaratibu na mpangilio wa uandishi wa ripoti kutoka utangulizi hadi hitimisho ni kipengele ambacho wengi walionekana kutofahamu. Watahiniwa wengine pia hawakuelewa jinsi ya kuendeleza mahojiano. Kuna uwezekano kuwa tatizo lilikuwa uelewa wa swali na kilichohitajika kwa maswali ya sampuli hizi mbili. Wengine waliendeleza mahojiano bila kutambua kwamba ni mazungumzo kati ya watu wawili au zaidi wala si hadithi ya kusimulia tu. Katika mada ya mahojiano, labda si wanafunzi wengi walielewa suala la usomaji wa lugha kwa mbali kutumia


International Baccalaureate
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

mitandao na tovuti. Swali lingine lililowatatiza wanafunzi ni lile lililohusu kuandika kwenye blogu. Huenda watahiniwa wengine hawakulielewa swali ipasavyo. Kulikuwa na utokaji kando wa mada miongoni mwa wanafunzi.

## Sehemu za programu na mtihani ambazo wanafunzi walionekana kuwa wemejitayarishia vyema

Uandishi wa barua ulionekana kuwa unaeleweka vizuri sana miongoni mwa wanafunzi wengi. Mada ya utamaduni na mtindo wa mavazi katika jamii sanasana miongoni mwa vijana iliwapendeza wengi na wakaichangamkia bila ugumu. Utangulizi, uendelezaji na jinsi ya kuhitimisha barua ni miongoni mwa mambo watahiniwa walionyesha umahiri wao. Hotuba pia ni insha ambayo wanafunzi wengi hawakutatizika sana nayo. Wanafunzi wana ufahamu wa kina wa masuala ya utamaduni na sherehe za kitaifa nchini. Jinsi ya kuandika hotuba kuzungumzia suala hili na kuweza kuendeleza mada yenyewe ilieleweka. Matumizi ya lugha na msamiati kulingana na mada ya insha yalikuwa mazuri na wengi waliweza kuandika kazi zenye mshikamano. Kuzingatia idadi ya maneno, watahiniwa waliweza kuandika kazi zenye urefu mwafaka na hoja za kina.

## Uwezo na udhaifu wa watahiniwa kwa maswali binafsi

Watahiniwa walionyesha uwezo wao wa lugha kwa kila swali, licha ya wakati mwingine kuonekana kupotoka na kutoka nje ya mada husika. Urefu wa kila kazi ulizingatiwa vizuri na karibu wanafunzi wote. Idadi ya maneno ilizingatiwa. Uwezo mkubwa ulionekana katika insha zilizohusu masuala ambayo wanafunzi wanashuhudia kila siku; kwa mfano: mtindo wa mavazi na sherehe za kitaifa. Uandishi wa barua na hotuba ni maarufu kwa wanafunzi wengi huku wengi wakiepuka insha zilizokuwa za muundo wa ripoti na mahojiano. Swali la kuandika ripoti kuhusu chakula kinachouzwa shuleni na uhusiano wake katika afya ya wanafunzi lilikwepwa na wengi, na miongoni mwa wachahche waliojaribu, kulikuwa na wasiojua utaratibu wa kuandika insha kama hii huku wengine wakipotoka kulingana na mada. Swali la mahojiano kuhusu mwanafunzi aliyejifundisha lugha kwa mbali pia liliwatatiza wengi. Jinsi ya kuandika mahojiano na mada yenyewe ni mambo mawili yaliyokuwa changamoto kwa wanafunzi.

## Mapendekezo na mwongozo wa kufundisha watahiniwa wa siku sijazo

Wanafunzi wanafaa kufundishwa kwa kina jinsi ya kuandika aina tofauti za insha; mpangilio, jinsi ya kuzienedeleza na vipengele muhimu vya kuzingatiwa katika uandishi huo; kwa mfano uandishi wa ripoti, mahojiano na blogu. Mazoezi ya kuandika insha kama hizi yangefaa kufanywa mara kwa mara ili wanafunzi wapate uzoefu wa kutosha na kufahamu muundo wake na jinsi ya kuendeleza insha za aina hii zilizo na kaida zake. Kipengele cha lugha kinachohusu upatanisho wa ngeli kinafaa kuangaliwa tena na tena. Kuna wanafunzi waliodhihirisha kutokuwa na msingi imara wa kutambua nomino ni ya ngeli gani na jinsi ya kuzingatia kanuni za upatanisho. Ni mazoezi tu na kusoma kwa kina katika upande wa wanafunzi kunakoweza kuboresha sarufi. Kwa jumla kazi za wanafunzi zilikuwa nzuri na walimu wao walikuwa wamewatayarisha vyema.


International Baccalaureate
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional